Jarida la

Ligi Kuu

Mei 2026



Unaikumbuka Mei 3?

Dakika 90 zilizoitingisha Tanzania

www.ligikuu.co.tz

Mwaka huu
utakuja nae au
utaomba VISA?

Usikubali kusimuliwa, jisajili sasa
tukutane Dodoma.

Jumapili » 26 Julai 2026



NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

NBC DODOMA MARATHON 2026

Tembelea **www.events.nbc.co.tz** Kuchangia

5KM » 10KM » 21KM » 42KM

Sanlam | Allianz

Yaliyomo

Kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu..... 1
Kariakoo Derby..... 3
Kona ya Ligi Kuu..... 8
Jicho la Kiufundi..... 12
'BOLI' na 'FASHENI'..... 19
Ligi ya Championship..... 22
First League..... 29
Ijue Kanuni..... 33







Kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu



Mwezi Mei umekuwa wa muhimu sana katika safari ya maendeleo ya Ligi Kuu ya NBC, Ligi ya Championship ya NBC na First League, ukiwa umebeba ushindani mkubwa ndani na nje ya uwanja. Tunajivunia kuona viwango vya ushindani vikiongezeka, ushirikiano wa wadau ukiendelea kuimarika, pamoja na mwitikio mkubwa wa mashabiki ambao ndio msingi wa mafanikio ya ligi zetu.

Kwa niaba ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, napenda kuzipongeza klabu zote kwa juhudi zao katika kuhakikisha ligi zinachezwa kwa weledi, nidhamu na ushindani wa hali ya juu. Aidha, tunathamini mchango wa wadhamini, vyombo vya habari,wamiliki wa viwanja na wadau wote wanaoshiriki katika kuendeleza soka la Tanzania.

Tunapoelekea hatua za mwisho za msimu, tunasisitiza umuhimu wa kuendelea kulinda misingi ya haki, uwazi, uadilifu na kufuata kanuni na Sheria zilizowekwa katika mashindano. Dhamira yetu ni kuhakikisha Ligi zetu zinaendelea kuwa jukwaa bora la kukuza vipaji, kuvutia uwekezaji na kuimarisha hadhi ya soka la Tanzania kimataifa.

Asanteni kwa kuendelea kuwa sehemu ya safari hii ya mafanikio. Kwa pamoja, tunaendelea kujenga ligi imara, zenye ushindani na thamani kubwa kwa taifa letu.

Cornel
Barnabas
Afisa Mtendaji Mkuu
Bodi ya Ligi Kuu Tanzania



Bodi ya Ligi Tuu Tanzania

Ghorofa na 14, NSSF Mafao House,
Barabara ya Uhuru - Ilala,
Dar es Salaam
S. L. P 79041 Dar es Salaam

www.ligikuu.co.tz
info@ligikuu.co.tz

Ligi Kuu

ligikuu | championshiptz | firstleague

tplboard

ligikuu

Ligikuu

LIGI KUU TV

Kariakoo ‘Derby’
Dakika 90 zilizoitingisha Tanzania

Kulikuwa na kila sababu ya kuisubiri Kariakoo ‘Derby’ ya Mei 3, 2026 iliyopigwa kwenye uwanja wa Mej. Jen. Isamuhyo, Dar es Salaam.

Siku chache kabla ya mchezo huo wa Ligi Kuu ya NBC, Tanzania ilikuwa imegawanyika katika rangi mbili nyekundu na kijani, Mitandao ya kijamii ilikuwa ya moto, Mijadala ilitawala kila kona ya nchi na mashabiki wa Simba walikuwa na ‘jeuri’ ya ushindi wao wa Kombe la Muungano Zanzibar walioupata huku Young Africans wakija na ‘ubabe’ wa kuwa vinara kwenye msimamo hivyo, Mei 3, haikuwa siku ya kawaida kwenye kalenda ya Ligi Kuu ya NBC.

Ilikuwa siku ambayo taifa lilikuwa linasubiri kuona nani angeandika historia mpya ya Kariakoo ‘Derby’ na mchezo ulipoanza haikuhitaji hata dakika tano kuonyesha ukubwa wake.

Simba maarufu kama ‘Mnyama’ aliingia uwanjani kama timu iliyokuwa na hasira, njaa ya ushindi na shauku ya kutuma ujumbe kwa wapinzani wao hao wakubwa kwamba sasa ubora wa timu yao umerejea na dakika za mwanzo zilikuwa kama dhoruba kwenye lango la Young Africans.

Mashambulizi yalifuatana kwa kasi kubwa na kabla mashabiki wengi hawajakaa vizuri kwenye viti vyao vya uwanja wa Isamuhyo winga wa Simba mzaliwa wa Senegal Libasse Gueye alikuwa tayari ameandika bao la kwanza lililodumu kwa dakika chache kabla ya ‘Mwamba wa Lusaka’ Clatous Chama kuongeza la pili kwa staili ambayo iliwafanya mamia ya mashabiki kusimama kwa mshangao.

Kwa muda huo, ilionekana kama Simba walikuwa wanaelekea kuandika moja ya ushindi mkubwa zaidi wa mchezo huo wa ‘watani wa jadi’ kwa hivi karibuni lakini Kariakoo ‘Derby’ huwa haiheshimu utabiri wa kutumia macho na ndani ya mchezo huu kuna vitu ambavyo havionekani kwenye takwimu navyo ni hisia kali, presha ya mchezo, historia ya timu hizi kongwe na kiburi cha utani wa jadi.

Young Africans maarufu kama ‘Wananchi’ walipoonekana kuyumba, walijikumbusha wao ni nani kwenye soka la Tanzania na zikisalia dakika chache kabla ya mpira kwenda mapumziko Prince Dube raia wa Zimbabwe akaanza safari ya kurejesha matumaini kwa mashabiki wa ‘Wananchi’ kwa kufunga bao lililobadilisha kabisa mwelekeo wa mchezo na ghafla uwanja ukabadilika, Sauti zikabadilika, Hofu ikaingia upande mmoja na matumaini yakahamia upande mwingine.

Kipindi cha pili kilianza huku kila upande ukifahamu mechi ilikuwa bado hai na yeyote atakayetumia nafasi zake vizuri atapata ushindi na ilikuwa timu ya Young Africans iliyorudi ikiwa na nguvu mpya na dakika chache baada ya kipindi cha pili kuanza nahodha wao Bakari Mwamnyeto akaandika bao la kusawazisha lililolipua furaha upande wa kijani na njano hivyo ‘Derby’ ikawa imeanza upya na dakika zilizobaki zikageuka kuwa vita ya mbinu, presha na mapambano ya kila mpira.

Kilichofanya mchezo huu kuwa maalum si matokeo ya 2-2 pekee bali ni namna ilivyobeba kila kitu ambacho mpira wa Tanzania unahitaji kuwa nacho ambacho ni mabao mazuri, presha ya 'utani wa jadi', nyota waliocheza kwa kiwango kikubwa, mashabiki waliotengeneza mandhari ya kipekee na hisia ambazo ni Kariakoo 'Derby' pekee inaweza kuzalisha.

Pengine picha kubwa zaidi ya mchezo huu ilikuwa namna ulivyovuta macho ya Afrika na dunia kwa bao la Clatous Chama lililoanza kusambaa kwenye majukwaa mbalimbali ya kimataifa huku mashabiki wengi wa soka wakilitaja kama moja ya mabao bora yaliyofungwa kwa mwaka huu na hata kwenye mijadala ya mashabiki wa soka duniani wengi walikuwa wakizungumzia ubora wa bao hilo na mazingira ya mchezo uliozalisha bao hilo.

Mwisho wa siku, hakuna aliyepata alama zote tatu lakini mpira wa Tanzania ulipata ushindi mkubwa, Ligi Kuu ya NBC ilipata ushindi mkubwa, Mashabiki walipata tamasha walilokuwa wakilisubiri na Kariakoo 'Derby' ikaendelea kuthibitisha kwa mara nyingine kuwa si mechi kubwa Tanzania pekee, bali ni 'derby' bora zaidi Afrika Mashariki na yenye hadhi kubwa zaidi Afrika hivyo kutuachia kumbukumbu moja muhimu sana kwamba huu si mchezo wa kuangaliwa tu bali ni tukio linaloishi mioyoni mwa mashabiki na kuandika historia mpya kila tarehe yake inapofika na kuendelea kuwa nembo kubwa ya ubora wa Ligi Kuu ya NBC na Ligi namba Sita kwa Ubora Afrika.



Nahodha wa timu ya Young Africans Bakari Mwamnyeto akishangilia bao lake la kusawazisha dhidi ya Simba.



Mchezaji wa timu ya Simba Clatous Chama akifunga bao kwenye mchezo wa Kariakoo Derby lililozua mjadala kwa namna yake ya ufungaji kwenye majukwaa mbalimbali ya habari duniani.



Yote kwa yote

ukiachana na upinzani unaokuwepo uwanjani mchezo huu umekuwa chachu ya kuleta upendo na kudumisha mahusiano baina ya mashabiki wa timu hizi.

Kona ya Ligi Kuu ya NBC

Msimu wa ‘moto’ Ligi Kuu ya NBC

MSIMU wa 2025/26 wa Ligi Kuu ya NBC umefika katika hatua ambayo kila mechi imekuwa na uzito wa fainali kuanzia juu ya msimamo wa ligi hadi chini kabisa kwenye eneo la kushuka daraja hakuna timu iliyobaki na nafasi ya kufanya makosa kwani huu ni msimu ambao umebeba ushindani mkubwa, presha kubwa na simulizi nyingi zilizoufanya kuwa miongoni mwa misimu yenye mvuto zaidi katika miaka ya hivi karibuni ya soka la Tanzania.



Mchezaji wa Young Africans Djigui Diarra (kushoto) akizungumza jambo na Libasse Gueye wa Simba (kulia) baada ya Kariakoo ‘Derby’kutamatika.

Mbio za ubingwa: ‘Vigogo’ wageuza Ligi Kuu ya NBC kuwa uwanja wa ‘Vita’

Msimu ulipoanza, wengi walitarajia ushindani wa kawaida kati ya timu za Young Africans na Simba pekee lakini kadri ligi ilivyoendelea ‘Matajiri wa Chamazi’ timu ya Azam walikataa kuendelea kubaki kama wapenzi watazamaji na leo hii vita ya ubingwa imekuwa simulizi kubwa zaidi ndani ya Ligi Kuu ya NBC.

Mabingwa watetezi, Young Africans wameendelea kuonyesha uthabiti mkubwa msimu mzima wakiwa wamekusanya jumla ya alama 60 katika michezo 25 waliyocheza na wakijiweka kileleni mwa msimamo kwa nguvu kubwa huku wakionyesha ubora mkubwa wa safu ya ushambuliaji yenye mabao 58 hadi sasa ikiwa kinara wa kufunga mabao na uimara wa safu ya ulinzi iliyoruhusu mabao tisa sawa na Azam huku zikiwa timu zilizoruhusu mabao machache.

Nyuma yao yupo ‘Mnyama’ Simba anayeendelea kufukuzia kwa kasi na kila ushindi anaopata ukiongeza ‘presha’ kwa wapinzani wao huku sare ya Kariakoo ‘Derby’ aliyopata, ushindi muhimu dhidi ya Dodoma Jiji na matokeo mengine ya hivi karibuni yamehakikisha mbio za ubingwa zinaendelea kuwa hai mpaka hatua za mwisho wa msimu.

Wakati huo huo Azam imekuwa hadithi nyingine kubwa ya msimu ambapo kwa muda mrefu walionekana kama timu ya kufuatilia tu mbio za ubingwa, lakini matokeo yao ya mara kwa mara yamewafanya waendelee kubaki karibu na nafasi za juu huku ushindi wao wa mabao 3-0 dhidi ya KMC ukionyesha wazi kuwa bado hawajakata tamaa katika vita hiyo.

Kilichofanya mbio hizi kuwa tamu zaidi ni kwamba hakuna timu inayotaka kulegeza mwendo na kila mechi imekuwa kama fainali hivyo kuongeza umakini kwa timu zote kwani kila kosa litakalofanyika linaweza kubadilisha taswira nzima yam bio za ubingwa.

Mbali na ubingwa kuna vita nyingine kali inayoendelea kimya kimya ya kuingia katika nafasi za uwakilishi wa kimataifa huku timu kadhaa zikiendelea kupambana kuhakikisha zinamaliza msimu katika nafasi zitakazowapa nafasi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye mashindano ya Afrika (CAF).

Singida Black Stars inashika nafasi ya nne ikiongoza mbio hizo baada ya kukusanya alama 40, ikifuatiwa kwa karibu na ‘Maafande’ wa JKT Tanzania wenye alama 38 wakishika nafasi ya tano na TRA United yenye maskani yake mkoani Arusha ikishika nafasi ya sita baada ya kukusanya alama 37.

Tofauti ya alama kati ya timu nyingi za juu imeendelea kuwa ndogo kiasi kwamba ushindi mmoja unaweza kukupeleka juu ya msimamo, huku kipigo kimoja kikakuondoa kabisa kwenye hesabu za uwakilishi wan chi kwenye mashindano ya Afrika na hii ndiyo sababu kila raundi ya mwisho ya msimu imekuwa ikiongeza joto zaidi kwenye ligi.

Vita ya Kusalia Kwenye Ligi sio ya ‘Kitoto’.

Kama juu kuna ndoto za ubingwa basi chini kuna mapambano ya



Mchezaji wa KMC Juma Shemvuni (kulia) akiwania mpira dhidi ya Jean Ngita wa Azam (kushoto) kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya NBC iliyochezwa uwanja wa Azam Complex, Dar.

kuendelea kula keki ya Ligi Kuu ya NBC kwa msimu unaofuata hivyo timu zinazopigania kusalia Ligi Kuu ya NBC kila dakika ya mchezo imekuwa na thamani kubwa sana ya kuhakikisha zinafanya yale yaliyo sahihi kwenye michezo yao.

Nafasi ya 11 hadi 15 zinatenganishwa na alama saba pekee hali inayofanya mbio za kujiokoa kuwa ngumu na za kusisimua zaidi kuliko wakati mwingine wowote msimu huu.

Timu ya Mashujaa ya Kigoma inayoshika nafasi ya 11 ikiwa na alama 27 bado haijawa salama kabisa licha ya kuwa na sare nyingi kuliko timu yoyote kwenye ligi bado inahitaji matokeo mazuri katika mechi zilizosalia ili kuondoa hofu ya kujikuta wakishuka kwenye eneo la hatari.

Mtibwa Sugar ya Morogoro inayoshika nafasi ya 12 baada ya kukusanya alama 27 pia inakabiliwa na presha kwani kikosi hicho kinafahamu kuwa ushindi mmoja unaweza kuwaweka salama ingawa matokeo mabaya yanaweza kukisukuma karibu zaidi na mstari wa kushuka daraja.

Nafasi ya 13 inashikwa na 'wauaji wa kusini' timu ya Namungo ya mkoani Lindi, iliyopo chini ya kocha wa zamani wa Simba Juma Mgunda yenye alama 25 huku tofauti ya alama na timu iliyopo kwenye nafasi ya kushuka daraja ikiwa ni tano pekee.

Mbeya City maarufu kama 'Purple Nation' ipo nafasi ya 14 baada ya kukusanya alama 22 ikiwa nafasi ya kucheza michezo ya mtoano wa kushuka endapo timu hiyo itamaliza msimu kwenye nafasi hiyo sawa na Namungo iliyopo nafasi ya 13.

Katika nafasi ya 15 timu ya 'Wajela jela' Tanzania Prisons imekusanya alama 20 na ipo ndani ya eneo la kushuka daraja huku ikiwa na tofauti ya alama mbili pekee dhidi ya majirani zao wa Mbeya City hali inayoonyesha kuwa bado wana nafasi ya kupambana na kusalia kwenye Ligi Kuu ya NBC msimu ujao.

Wakati huo huo vijana wa 'Kino Boys' timu ya KMC iliyopo mkiani mwa msimamo na alama 9 inakabiliwa na kazi ngumu zaidi ya kujiokoa na kushiriki Ligi ya Championship ya NBC msimu ujao kwani endapo itapoteza mchezo wake unaofuata itakuwa imeshuka daraja rasmi.

Kwa mechi tano zilizosalia kwa kila timu, vita ya kusalia Ligi Kuu ya NBC imeingia katika hatua ya mwisho yenye msisimko mkubwa ambapo kila alama, kila bao na kila dakika inaweza kuamua hatima ya timu hizo msimu huu endapo zitakuwepo kwenye Ligi Kuu ya NBC au zitakuwa wageni wa Ligi ya Championship ya NBC msimu wa 2026/27.




Wachezaji wa Mtibwa Sugar wakishangilia moja ya bao lao walilofunga kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya NBC mwezi Mei.



Jicho la Kiufundi

Na **Sisti Martin** sistinho


Mei 2026, Mwezi usiosahaulika kwenye 'Diary' za Fiesal, Chama na Okello,



Mabao-7
Pasi za Mabao-1



Mabao - 5
Pasi za Mabao-4



Mabao - 9
Pasi za Mabao-1

Wametikisa takwimu za Ligi

Kati ya jumla ya magoli 121 yaliyofungwa kwenye mechi 45 za Ligi kuu ya NBC ndani ya mwezi huo, Magoli 27 yamechangiwa na nyota hao watatu tu ambayo ni sawa na asilimia 37.2%

MMwezi Mei 2026, unaweza kuwa mwezi bora zaidi kwenye msimu huu kwa wachezaji watatu nyota wa Ligi kuu ya NBC (NBC Premier League) Feisal Salum wa Azam FC, Clatous Chama wa Simba SC na Allan Okello wa Yanga SC ambao wameonyesha kiwango cha juu kwenye mwendelezo bora kwa mwezi mzima.

Wanatumiwa vipi Kimbinu?

Wachezaji hao wote watatu kwa pamoja hutumiwa kama viungo washambuliaji wa kati, nyuma ya mshambuliaji wa mwisho kwenye mifumo ya uchezaji inayofanana, ambapo;

Feisal, kwenye mbinu za Florent Ibenge pale Azam FC mara nyingi hucheza nyuma ya Kitambala Bola kwenye mfumo wa 4-2-3-1, ambapo wakati wa kuzuia huwa usawa wa mshambuliaji huyo raia wa Congo DR kwenye muundo wa 4-4-2.

Okello, kwenye mbinu za Abdihamid Moallin pale Yanga SC mara nyingi hucheza nyuma ya Prince Dube kwenye mfumo wa 4-2-3-1, ambapo wakati wa kuzuia huwa usawa wa mshambuliaji huyo raia wa Zimbabwe kwenye muundo wa 4-4-2.

Chama, kwenye mbinu za Steve Berker pale Simba SC mara nyingi hucheza nyuma ya Ellie Mpanzu kwenye mfumo wa 4-2-3-1, ambapo wakati wa kuzuia huwa usawa wa mshambuliaji huyo raia wa Congo DR kwenye muundo wa 4-4-2.

Chama, kwenye mbinu za Steve Berker pale Simba SC mara nyingi hucheza nyuma ya Ellie Mpanzu kwenye mfumo wa 4-2-3-1, ambapo wakati wa kuzuia huwa usawa wa mshambuliaji huyo raia wa Congo DR kwenye muundo wa 4-4-2.
Namna walivyozipa timu zao Magoli na Asisti
Makala hii inaonyesha namna ambavyo uwezo wa kiufundi na uelewa wa kimbinu wa wachezaji hawa umeweza kuwa mwiba mkali kwa wapinzani wao kiasi cha kuweza kuweka historia hizo;

Feisal Salum



Feisal ameonyesha hatari zaidi wakati wa mipira ya kutenga (Set Pieces) ambapo kati ya magoli 8 aliyochangia Feisal kwa mwezi Mei (Goli 7 na Asisti 1), magoli mawili (dhidi ya Mtibwa Sugar na Pamba Jiji) yametokana na ubora wake wa kushambulia nafasi kwenye boxi wakati wa kona na kufunga kwa kichwa huku magoli mawili akifunga kwa mikwaju ya penalti)

Pia Feisal ameonyesha ubora kwenye upishi na umaliziaji wa kona mkubwa wakati wa timu yake ikiwa na mpira (In Possession) kwenye eneo la mwisho la wapinzani ambapo ameweza kutoa asisti ya goli dhidi ya Mtibwa Sugar kwa krosi kali huku yeye pia akifunga kwa kichwa akimalizia krosi kwenye mchezo dhidi ya KMC.

Kwenye mashambulizi ya kujibu pindi Azam FC inapopora mpira (Positive Transitions) Feisal ameonekana kuwa silaha muhimu kushambulia nafasi nyuma ya washambuliaji wake ambao hupokea mipira kutoka nyuma wakiwa kwenye shinikizo la wapinzani na kutengeneza nafasi kwake, mfano ni goli dhidi ya KMC.



Allan Okello

Kati ya mabao 10 aliyochangia kwa mwezi Mei, Okello amefunga mabao matano na kutoa pasi moja ya bao pindi Young Africans inapokuwa na mpira (In Possession) ambapo amekuwa hatari kushambulia nafasi nyuma ya viungo wa timu pinzani nje ya 18 (Zone 14) mfano mchezo dhidi ya KMC na Coastal Union na hata Singida aliweza kufunga kutoka eneo hilo kwa mpira wa madhambi (Set Play hasa Freekick).
Pia nyota huyo amekuwa hatari kushambulia kwenye nafasi kati ya walinzi wa kati na wa pembeni (Half Spaces) mfano kwenye mechi dhidi ya Coastal Union ambapo alitoa pasi ya bao kwa Maxi Nzengeli kutoka kwenye eneo hilo.

Mara nyingine nafasi nyuma ya walinzi hasa kwenye mashambulizi ya kujibu pindi Young Africans inapochukua mpira na kushambulia kabla wapinzani wao hawajarejea kwenye muundo wao mzuri wa kuzuia (Positive Transitions) mfano kwenye mechi dhidi ya Dodoma Jiji.



Clatous Chama

Kati ya mabao tisa aliyochangia kwenye mwezi Mei, Mabao sita ya Chama yametokea wakati wa mashambulizi ya kujibu (Positive Transitions) yaani Simba walikuwa wakizuia na kumshinikiza mpinzani kukosea ili waibe mpira na kujibu shambulizi, ambapo Chama amefunga mabao matatu kwa kushambulia nafasi baada ya Simba kupora mpira, mfano ni mabao dhidi ya Young Africans, JKT Tanzania, Mashujaa na Tanzania Prison huku yeye mwenyewe akipika mawili dhidi ya Coastal Union na Tanzania Prisons.

Mabao matatu kati ya aliyoyafunga yamepikwa na Elie Mpanzu ambaye amekuwa akisimama naye kwenye mstari wa mbele wa uzuiaji, Mara baada ya kupora mpira wote hushambulia nafasi kwa haraka, mmoja akiwa na mpira mwingine akishambulia nafasi.

Mabao matatu yaliyobaki ameyachangia wakati wa mipira ya kutenga (Set Pieces) ambayo yote ni ya kona, akitoa pasi za mabao mawili dhidi ya Tanzania Prison na Coastal Union na yeye akifunga kwa kona ya moja kwa moja dhidi ya Mashujaa FC.

Tujivunie uwepo wao kwenye Ligi yetu

Kinda tishio anayekuja kwa kasi Ligi Kuu ya NBC

Kila msimu wa Ligi Kuu ya NBC, kuna nyota wengi wapya wenye umri mdogo wanaong'ara ambao ni wale wanaotoka kimya kimya, wanaocheza bila presha kubwa ya kuwa na majina makubwa, halafu ghafla wanalazimisha kila mtu awaangalie kila mchezo wao unapofika.

Mwezi Mei wa Ligi Kuu ya NBC ulikuwa mwezi wa aina hiyo kwa nyota Henry David wa kikosi cha Fountain Gate.

Wakati macho ya mashabiki wengi yalikuwa kwa nyota wa timu kubwa zinazowania ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC, Henry David alikuwa akijenga simulizi yake mwenyewe taratibu na kimya kimya lakini kwa ubora uliokuwa unaonekana wazi kabisa ndani ya uwanja.

Fountain Gate walikuwa na mwezi mgumu wenye mechi za ushindani mkubwa, lakini katika kipindi hicho timu ilionyesha ushindani mkubwa kwa kushinda michezo muhimu dhidi ya Coastal Union, KMC na TRA huku ikipata matokeo mengine muhimu yaliyoiweka kwenye nafasi nzuri ya kuendelea kupambana ndani ya Ligi Kuu ya NBC.

Katikati ya safari hiyo, jina la Henry David raia wa Nigeria likaanza kujitokeza mara kwa mara na katika ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Coastal Union, Henry David alifunga bao muhimu lililoonyesha utulivu, ujasiri na uwezo mkubwa wa kusoma mchezo licha ya umri wake mdogo bao lililokuwa moja ya alama zilizothibitisha kuwa kijana huyo si mchezaji wa kawaida ndani ya kikosi cha Fountain Gate.

Kilichovutia zaidi mwezi huu halikuwa bao hilo dhidi ya Coastal bali alifanikiwa kufunga bao lingine zuri kwenye uwanja wa KMC Complex akitumia uwezo binafsi wa kukokota mpira kuanzia kati ya uwanja hadi eneo la hatari na kuonyesha ufundi wa kuitoka ‘ngome’ ya ulinzi dhidi ya mabeki wa KMC.

Uwezo wa kinda huyu mwenye miaka 20 haujathibitika kwa mabao anayofunga pekee bali kwa namna anavyocheza kwa kusumbua mabeki wa upande wa upinzani, namna anavyojituma, namna anavyoingia kwenye mapambano ya mpira na namna anavyokuwa tayari kubeba majukumu makubwa wakati timu yake inapomuhitaji.

Katika kipindi ambacho Fountain Gate walikuwa wakitafuta matokeo muhimu, Henry David alikuwa mmoja wa wachezaji waliokuwa wakionyesha uthubutu mkubwa kila wanapopewa nafasi na takwimu za timu zinaonyesha kuwa tayari amejiweka miongoni mwa wafungaji wanaoongoza ndani ya kikosi cha Fountain Gate akishika nafasi ya tatu hadi sasa msimu huu akifunga jumla ya mabao matatu nyuma ya Chukunonye Obasi mwenye sita na Ismail Aziz mwenye tano jambo linaloonyesha mchango wake mkubwa kwenye safu ya ushambuliaji ya timu hiyo.

Zaidi ya takwimu, kuna jambo ambalo haliwezi kupimwa kwa namba nalo ni athari yake ndani ya mchezo kila anapokuwa na mpira na kila anapokaribia eneo la hatari la wapinzani kuna matarajio kutoka kwa mashabiki kwamba anaweza kuwanyanyua kwenye viti muda wowote jambo ambalo linamtenganisha na ‘chipukizi’ wengine wanaokuja kwa kasi kwenye Ligi Kuu ya NBC.

Ndiyo maana, ukiangalia mchango wake kwa timu yake, maendeleo yake na kiwango alichoonyesha mwezi Mei ni vigumu kuzungumzia chipukizi bora wa mwezi bila kulitaja jina la Henry David wa Fountain Gate.





Miaka 20

Jina: **Henry David**

Nafasi: **Kiungo Mshambuliaji**

Uraia: **Nigeria**

Tarehe ya Kuzaliwa: **Machi 5, 2006**

miaka: **20**

Timu: **Fountain Gate**

Vinara wa takwimu Ligi Kuu ya NBC mwezi Mei, 2026

Kinara wa Mabao

ALLAN OKELLO

Michezo	6
Dakika	509
Mabao	9



Kinara wa Hati safi



MAHAMADOU KASSAL

Michezo	6
Dakika	540
Hati Safi	4
Mabao Aliyoruhusu	3

Kinara wa Pasi Saidizi

CLATOUS CHAMA

Michezo	6
Dakika	500
Pasi za Mabao	4



Kinara wa Kuhusika kwenye Mabao



ALLAN OKELLO

Michezo	6
Dakika	509
Mabao	9
Pasi za Mabao	1
Mabao Aliyohusika	10

Omary Marungu



‘BOLI’ & ‘FASHENI’





Ahmad Ally



NBC CHAMPIONSHIP LEAGUE

championshiptz



Kagera Sugar,Geita Gold

Hakuna mbabe msimu wa 2025/2026

MEI 23, 2026 uwanja wa Kaitaba mkoani Kagera ulikuwa ‘kitovu’ cha hisia za mashabiki wa soka wakati ‘vigogo’ wa NBC Championship, Kagera Sugar na Geita Gold walipokutana katika mchezo uliokuwa ukisubiriwa kwa hamu kubwa ambapo licha ya dakika 90 za ushindani mkali mchezo huo ulimalizika kwa sare ya bila kufungana huku katika mchezo wa mzunguko wa kwanza timu hizo zilipokutana kwenye uwanja wa Nyankumbu mkoani Geita matokeo yakiwa ni sare ya 1-1.

Mchezo huo uliwapa mashabiki kila kitu walichotarajia kutoka kwa timu mbili bora zaidi za NBC Championship msimu huu ambapo kulikuwa na mapambano ya nguvu, nidhamu ya hali ya juu, mbinu za makocha na ari kubwa ya kutafuta ushindi ambao ungeweza kubadilisha mwelekeo wa mbio za kupanda Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/27.

Chini ya kocha Juma Kaseja timu ya Kagera Sugar iliyokuwa nyumbani ilitumia mchezo huo kama fursa ya kupunguza pengo dhidi ya vinara Geita Gold na mashabiki wao walijitokeza kwa wingi wakiamini timu yao ingeweza kutumia faida ya uwanja wa nyumbani kupata alama tatu muhimu, hata hivyo, walikutana na Geita Gold waliokuja wakiwa na dhamira ya kulinda nafasi yao kileleni na kuhakikisha hawapotezi mchezo.

Kwa upande wa Geita Gold, sare hiyo ilionekana kuwa matokeo yenye thamani kubwa na kuondoka Kaitaba bila kupoteza dhidi ya mpinzani wao mkubwa wa moja kwa moja ni ishara ya ukomavu wa kikosi hicho chini ya kocha Zuberi Katwila ambacho kwa muda mrefu kimeonyesha ukomavu wa hali ya juu katika mbio za kurejea Ligi Kuu.

Mbali na kuwa timu hizi zinachuana vikali kileleni, kwenye upande wa vinara wa ufungaji wa mabao bado ni wachezaji wa timu zao wapo nafasi ya kwanza na ya pili ambapo Obrey Chirwa anashikilia usukani wa ‘kucheka na nyavu’ akifunga mabao 16 huku Maulid Shaban wa Geita akiwa nafasi ya pili baada ya kufunga mabao 14.



‘Vigogo’ wanaowania ubingwa wa Ligi ya NBC ya Championship

Baada ya michezo 27 ya msimu, Geita Gold wanaendelea kuongoza msimamo kwa alama 68 huku Kagera Sugar wakifuatia kwa alama 65 wakipishana kwa alama tatu pekee, hali inayoonyesha namna ushindani ulivyo mkali na kwa nini pambano lao la Kaitaba lilikuwa na umuhimu mkubwa.

Geita Gold wamekuwa timu ya mfano msimu huu wakiwa na ushindi kwenye michezo 21 kati ya 27 na wameonyesha mchanganyiko wa safu kali ya ushambuliaji na ulinzi imara wakifunga mabao 60 yakiwa mengi zaidi kwenye ligi jambo linaloonyesha uwezo wao mkubwa wa kutumia nafasi wanazopata kuwa mabao.

Kagera Sugar nao wamekuwa na msimu wa kuvutia sana wakishinda michezo 20 hadi sasa hali inayoonyesha jinsi walivyoweza kuhimili presha ya ligi na kuendelea kuwa karibu na usukani wa ligi huku uzoefu wao mkubwa katika soka la ushindani ukionekana wazi katika mechi nyingi walizocheza msimu huu.

Matokeo ya sare ya 0-0 Kaitaba yanaweza yasionekane makubwa kwenye karatasi lakini athari yake katika mbio za ligi ni kubwa sana kwani Geita wameendelea kubaki kileleni huku wakihifadhi tofauti yao dhidi ya Kagera Sugar wakati Kagera nao wameendelea kushikilia nafasi ya pili na kujiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea kupigania tiketi ya kupanda daraja.

Kwa hatua ambayo msimu umefikia kila alama ina thamani ya ‘dhahabu’ na hakuna timu inayoweza kumudu kufanya makosa makubwa katika michezo iliyosalia kwani ushindani kutoka kwa Polisi Tanzania na Mbeya Kwanza bado unaonyesha endapo ‘vigogo’ hao watakosa matokeo mazuri kwa michezo inayofuata nafasi yao kupanda Ligi Kuu ya NBC itakuwa matatani.

Safari bado haijaisha, lakini baada ya sare ya Kaitaba, Geita Gold na Kagera Sugar wameendelea kuthibitisha kuwa wao ndio wahusika wakuu wa simulizi la msimu huu, simulizi la ushindani, uthabiti na ndoto ya kurejea kwenye jukwaa kubwa zaidi la soka la Tanzania.



‘Macho kodo’ kuelekea mwisho wa msimu NBC Championship.

Msimu wa NBC Championship 2025/26 umefikia hatua ambayo kila mchezo una uzito wa kipekee ambapo wakati timu zinazowania kupanda Ligi Kuu ya NBC zikiongeza kasi kuelekea kufanikisha malengo yao upande wa chini wa msimamo nao ushindani umegeuka kuwa vita ya kuokoa maisha ya klabu kuhakikisha zinasalia kwa msimu ujao.

Baada ya mzunguko wa 27 wa NBC Championship picha ya msimu imeanza kuwa wazi na baadhi ya timu zimeonyesha uimara tangu mwanzo wa msimu huku nyingine zikijikuta zikilazimika kupigania malengo yao hadi dakika za mwisho kuhakikisha zinakuwa sehemu ya NBC Championship.

Na	Timu	P	W	D	L	GF	GA	GD	PTS
1	Geita Gold	27	21	5	1	60	15	45	68
2	Kagera Sugar	27	20	5	2	49	12	37	65
3	Polisi Tanzania	27	18	6	3	47	19	28	60
4	Mbeya Kwanza	27	18	3	6	51	24	27	57
5	Transit Camp	27	15	5	7	38	28	10	50
6	Mbuni	27	14	2	11	36	27	9	44
7	Gunners	27	11	5	11	31	37	-6	38
8	Kengold	27	9	6	12	29	38	-9	33
9	Bigman	27	8	8	11	26	27	-1	32
10	B19	27	8	7	12	24	38	-14	31
11	TMA	27	8	6	13	21	29	-8	30
12	Songea United	27	7	8	12	23	35	-12	29
13	Stand United	27	8	4	15	24	39	-15	25
14	African Sports	27	5	2	20	23	51	-28	17
15	Barberian	27	1	9	17	15	41	-26	12
16	Hausung	27	3	3	21	16	53	-37	9



Msimamo wa Ligi ya NBC Championship, na mbio za kurejea Ligi kuu ya NBC

Kinara wa msimamo wa Ligi ya Championship ya NBC timu ya Geita Gold imeendelea kuonyesha dhamira ya kurejea Ligi Kuu ya NBC baada ya kukusanya alama 68 katika michezo 27 ikishinda 21, sare tano na kupoteza mchezo mmoja pekee ikiwa na takwimu zinazothibitisha ubora wa kikosi hicho msimu huu.

Geita Gold wamekuwa na safu kali ya ushambuliaji iliyofunga mabao 60 huku wakiruhusu mabao 15 jambo linalowaweka katika nafasi nzuri ya kutimiza ndoto yao ya kurejesha michezo ya Ligi Kuu ya NBC kwenye ‘Dimba’ la Nyankumbu mkoani Geita hivyo kutimiza hilo watahitajika kuendelea kupata matokeo mazuri na endapo itafanikiwa kupata alama moja kwenye mchezo wake basi rasmi itakuwa imekata tiketi ya kushiriki Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/27.

Kama kuna timu ambayo imekuwa ikiifanya Geita Gold isiwe na amani kwenye nafasi yake basi ni ‘Wakata Miwa’ wa Kagera Sugar wenye alama 65 ikiwa ni tofauti ya alama tatu pekee dhidi kinara hali inayoonyesha kuwa mbio za ubingwa wa NBC Championship bado hazijafika tamati.

Kagera Sugar wameonyesha ubora msimu huu kwa kushinda michezo 20 kati ya 27 waliyocheza huku kikosi hicho kikiendelea kuthibitisha kuwa kina uzoefu wa kushindana katika mazingira ya presha kubwa na kusalia kuwa miongoni mwa timu zinazopewa nafasi kubwa ya kurejea Ligi Kuu ya NBC msimu ujao.

Katika nafasi ya tatu na nne timu ya Polisi Tanzania na Mbeya Kwanza wanaendelea kufukuzia nafasi za juu zinazoweza kuwapeleka kwenye hatua za mtoano ili kuweza kupanda daraja.

Polisi Tanzania wana alama 60 huku Mbeya Kwanza wakifuatia na alama 57 ingawa tofauti kati yao na timu mbili za juu imeongezeka huku bado michezo iliyobaki inaweza kubadilisha hesabu zote na kuwafanya waweze kupanda daraja.

Kwa timu hizi, lengo kubwa sasa ni kuhakikisha zinamaliza msimu katika nafasi zinazowapa fursa ya kuendelea kupigania tiketi ya kupanda Ligi Kuu na kuhakikisha hawaruhusu timu za chini kuwapiku kwenye nafasi hiyo.

Transit Camp wamekuwa miongoni

mwa timu zilizovutia msimu huu kwa kukusanya alama 50 na kuonyesha ushindani mkubwa dhidi ya vigogo wa ligi huku timu ya Mbuni kutoka mkoa wa Arusha ikiendelea kuwa wapinzani wagumu licha ya kushindwa kuingia kwenye mbio za moja kwa moja za kupanda daraja.

Transit Camp na Mbuni ndio timu pekee ambazo zina uhakika wa kutokucheza michezo ya mtoano hivyo zitasalia NBC Championship lakini timu za Gunners, Kengold, Bigman na B19 zimeunda kundi la timu ambazo kwa kiasi kikubwa hazijapata uhakika wa kuwa sehemu ya ligi hiyo kwa msimu ujao.

Kwa timu hizi kila mchezo uliosalia ni nafasi ya kujizatiti na kuongeza thamani ya klabu na kuweka msingi mzuri wa msimu ujao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha zinaendelea kukusanya alama muhimu ili kuepuka kushuka nafasi ya chini na kumaliza msimu vibaya.

mwa timu zilizovutia msimu huu kwa kukusanya alama 50 na kuonyesha ushindani mkubwa dhidi ya vigogo wa ligi huku timu ya Mbuni kutoka mkoa wa Arusha ikiendelea kuwa wapinzani wagumu licha ya kushindwa kuingia kwenye mbio za moja kwa moja za kupanda daraja.

Transit Camp na Mbuni ndio timu pekee ambazo zina uhakika wa kutokucheza michezo ya mtoano hivyo zitasalia NBC Championship lakini timu za Gunners, Kengold, Bigman na B19 zimeunda kundi la timu ambazo kwa kiasi kikubwa hazijapata uhakika wa kuwa sehemu ya ligi hiyo kwa msimu ujao.

Kwa timu hizi kila mchezo uliosalia ni nafasi ya kujizatiti na kuongeza thamani ya klabu na kuweka msingi mzuri wa msimu ujao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha zinaendelea kukusanya alama muhimu ili kuepuka kushuka nafasi ya chini na kumaliza msimu vibaya.





Vita ya kusalia kwenye Ligi ya Championship ya NBC

Chini ya msimamo ndipo penye ‘sinema’ zaidi kwa sasa kwani timu ya TMA iliyopo nafasi ya 11 baada ya kukusanya alama 30 na Songea United yenye alama 29 katika nafasi ya 12 bado hazipo salama zikiwa na tofauti ndogo ya alama kati yao na timu zilizo chini, ikimaanisha kuwa makosa machache yanaweza kuwavuta kwenye eneo la hatari.

Stand United inashika nafasi ya 13 ikiwa na alama 25 ikiwa timu ya pili kwa kupata sare nyingi msimu huu (8) sawa na Bigman ikiwa imepoteza michezo 15 hadi sasa huku ikiwa mbele ya mstari wa kushuka daraja kwa alama 12.

African Sports iliyopo nafasi ya 14 baada ya kuvuna alama 17 inakaribia kujihakikishia nafasi ya kucheza hatua ya mtoano ikiwa itafanikiwa kupata ushindi kwenye michezo yake miwili inayofuata

Chini ya msimamo ndipo penye ‘maigizo’ zaidi kwa sasa kwani timu ya TMA iliyopo nafasi ya 11 baada ya kukusanya alama 30 na Songea United yenye alama 29 katika nafasi ya 12 bado hazipo salama zikiwa na tofauti ndogo ya alama kati yao na timu zilizo chini, ikimaanisha kuwa makosa machache yanaweza kuwavuta kwenye eneo la hatari.

Stand United inashika nafasi ya 13 ikiwa na alama 25 ikiwa timu ya pili kwa kupata sare nyingi msimu huu (8) sawa na Bigman ikiwa imepoteza michezo 15 hadi sasa huku ikiwa mbele ya mstari wa kushuka daraja kwa alama 12.

African Sports iliyopo nafasi ya 14 baada ya kuvuna alama 17 inakaribia kujihakikishia nafasi ya kucheza hatua ya mtoano ikiwa itafanikiwa kupata ushindi kwenye michezo yake miwili inayofuata

ikikosa nafasi ya kusalia kwenye Ligi ya Championship ya NBC bila kucheza hatua ya mtoano kutokana na uwiano wa alama na timu za juu kuwa mkubwa.

Katika eneo la kushuka daraja moja kwa moja timu za Barberian na Hausung zinakabiliwa na presha kubwa zaidi huku zikihitaji ‘Dua’ nyingi ili kusalia kwenye ligi msimu ujao baada ya kukabiliwa na muendelezo wa matokeo mabaya yanayofanya nafasi zao za kubaki kuwa finyu.

Barberian wana alama 12 baada ya michezo 27 wakiwa nyuma ya African Sports kwa alama tano huku matumaini ya kusalia kwenye ligi yakiwepo lakini kwa upande wa Hausung yenye alama tisa itakuwa ikipiga ‘maombi’ ya kiwango cha juu kwani endapo African Sports itashinda mchezo wake unaofuata basi moja kwa moja timu hiyo itakuwa imeshuka daraja.

First League

firstleaguetz

Hatua za mwisho za First League ‘usipime’



Rangers ikimaliza safari yake kwenye kundi B baada ya kufanikiwa kupanda daraja ikikusanya alama ambazo haziwezi

MSIMU wa First League 2025/26 unaendelea kushika kasi huku Makundi A na B yakishuhudia ushindani mkubwa wa kuwania nafasi za kupanda Ligi ya Championship ya NBC na kuepuka kushuka daraja baada ya michezo 12 kwa kila timu huku Bandari Tanzania ikiendelea kuonyesha ubora wa hali ya juu na kushikilia usukani wa kundi A huku Rhino Rangers ikimaliza safari yake kwenye kundi B baada ya kufanikiwa kupanda daraja ikikusanya alama ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote.

Bandari mguu mmoja ndani NBC championship.

Bandari wamejijengea mafanikio kupitia mchanga-nyiko wa safu imara ya ushambuliaji na ulinzi wakifunga mabao 22 na kuruhusu mabao saba pekee hadi sasa wakiwa wameonyesha kwa vitendo kuwa hawapo kileleni kwa bahati mbaya wakipata ushindi kwenye michezo tisa katika michezo 12 na kuweka mfukoni jumla ya alama 29.

Hata hivyo, safari bado ni ndefu kwani timu ya Nyumbu inaendelea kuwafuatilia kwa karibu wakiwa na pointi 23 licha ya kushinda michezo sita pekee na kupata sare tano zilizowasaidia kusalia kwenye nafasi za juu na kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kuwania nafasi ya kucheza hatua za mtoano za kupanda NBC Championship.

Cosmopolitan nao wameendelea kuwa tishio wakiwa nafasi ya tatu baada ya kukusanya alama 22 wakionyesha uwezo mkubwa wa kufunga mabao huku wakibeba matumaini baada ya kujiweka kwenye nafasi ya kupanda NBC Championship kupitia hatua ya mtoano kwani hata wakipoteza michezo yao iliyosalia bado watakuwa katika nafasi waliyopo sasa.

Wakati timu za juu zikihangaikia ndoto za kupanda daraja hali si shwari kwa upande wa chini wa msimamo kwani timu za Dar City na Green Warriors wote wamekusanya pointi 11 baada ya mechi 12 na wanakabiliwa na hatari ya kucheza hatua za mtoano, lakini endapo watashinda michezo yao miwili watafanikiwa kujinasua kwenye nafasi ya kucheza hatua ya mtoano.

Mateso makubwa zaidi kwa sasa yanawakabili Pan African ambao wamesalia mkiani mwa msimamo kwa alama tisa pekee wakishinda michezo miwili kwenye michezo 12 hali inayowaweka kwenye mazingira magumu na ikiwa wanahitaji kusalia kwenye First League msimu ujao wanatakiwa kuhakikisha wanapata ushindi kwenye michezo yao iliyosalia na kuombea Dar City au Green Warrior wapotezo moja ya michezo yao.





Rhino ‘walee’ NBC championship

Upande wa kundi B ‘kesi’ ya nani atapanda NBC Championship imekwisha kupata ufumbuzi baada ya Rhino Rangers kujihakikishia nafasi hiyo ikikusanya alama 31 ambazo hazitaweza kufikiwa na timu nyingine yoyote baada ya michezo 12 kwa kila timu.

Rhino Rangers wamekuwa katika kiwango cha juu tangu kuanza kwa msimu huu wakishinda mechi 10 kati ya 12 walizocheza huku timu hiyo ikionyesha uimara mkubwa katika kila eneo la timu huku mabao 29 waliyofunga yakiwa ndio mengi zaidi kwenye kundi na safu yao ya ulinzi ikiruhusu mabao tisa pekee yakiwa machache kuliko timu yoyote

IAA wanashika nafasi ya pili kwa alama 24 wakijihakikishia kupanda daraja kwa njia ya mtoano baada ya kushinda michezo saba wakihitaji kushinda michezo yao ili kumaliza msimu kwenye ari ya juu na kuuendea mchezo wa hatua ya mtoano.

Nafasi ya tatu inashikiliwa na Endument yenye alama 20 wakihitaji alama mbili ili kujihakikishia nafasi ya kucheza mchezo wa hatua ya mtoano wa kupanda daraja

Katikati ya msimamo timu za NKIM na Alliance zimekusanya alama 15 na kuendelea kusaka ushindi huku wakihitaji kushinda michezo yao miwili yote ili kujihakikishia nafasi ya kusalia kwenye First League msimu ujao

Chini ya msimamo kwenye nafasi za kucheza hatua ya mtoano kuna timu za Copco nafasi ya sita na Mapinduzi ya saba wakikabiliwa na presha ya kujinusuru na hatari ya kushuka daraja ambapo kila mchezo ukiwa muhimu kwao na endapo watashinda michezo yao miwili yote na timu za juu zikapoteza basi watakuwa nafasi nzuri sana ya kusalia kwenye ligi hiyo.

‘Wanajeshi wa mpakani’ timu ya Biashara United kutoka Mara ambayo iliwahi kucheza kwenye Ligi Kuu ya NBC imeshashuka daraja ikiwa na deni la alama nne baada ya kukatwa alama wakicheza michezo 12 bila kupata ushindi kwenye mchezo wowote wakifunga mabao manne na kuruhusu mabao 26’

Hawa hapa wageni wa First League 2026/27





Baada ya miezi ya mapambano, kujituma na kuamini ndoto zao timu ya Kajuna kutoka Kigoma na Kahama Madini ya Shinyanga zimeandika historia mpya kwa kufuzu kucheza Ligi ya First League msimu wa 2026/27 ikiwa ni mafanikio yaliyopatikana baada ya timu hizo kufanya vizuri katika Ligi ya Mabingwa wa Mikoa (RCL) na kufika hatua ya fainali jambo lililowapa tiketi ya moja kwa moja ya kupanda daraja.

Safari ya Kajuna imekuwa ya kuvutia zaidi wakiwa wenyeji wa michuano hiyo mkoani Kigoma wakionyesha mashabiki wao kandanda la kiwango cha juu ikiwemo ushindi mnono wa 8-0 dhidi ya Mount Hanang katika mchezo wa nusu fainali, ushindi uliodhihirisha ubora, umoja na njaa ya mafanikio waliyoonyesha tangu hatua za awali za mashindano hadi kufanikiwa kupanda daraja.

Kwa upande wa Kahama Madini, walionyesha ushujaa baada ya kuwa nyuma kwa bao dhidi ya Stand Masasi lakini hawakukata tamaa na walirejea na kushinda mabao 2-1, ushindi uliowahakikishia nafasi ya kucheza First League msimu ujao huku uwezo wao wa kupambana hadi dakika za mwisho ubeba taswira ya timu iliyojengwa kwa nidhamu, uvumilivu na malengo makubwa.

Kufuzu kwa hizi timu fainali kuliwapa tiketi ya moja kwa moja kushiriki First League msimu ujao ingawa Kajuna ndiye aliyeibuka bingwa wa ‘wababe’ wa mikoa kwa kuifunga Kahama Madini 2-0 kwenye mchezo wa fainali uliopigwa uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma na kuhakikisha ubingwa unasalia kwenye ardhi yao ya nyumbani.

Kupanda kwa Kajuna na Kahama Madini si mafanikio ya wachezaji na benchi la ufundi pekee, bali ni ushindi wa mikoa ya Kigoma na Shinyanga ambayo imeendelea kuwekeza katika maendeleo ya soka huku mashabiki wao wakiwa sehemu muhimu ya safari hii kwa kushangilia na kusimama na timu zao katika nyakati zote.

Macho yanaelekezwa First League ambapo changamoto zitakuwa kubwa zaidi tofauti na mechi za mabingwa wa mikoa lakini kwa namna walivyopambana kutoka ngazi ya RCL hadi kufikia hatua hii timu za Kajuna na Kahama Madini zimeonyesha kuwa hazijapanda daraja kwa bahati bali kwa juhudi, ubora na dhamira ya kufika mbali zaidi.



Zijue Kanuni



Kanuni: 17 (58)

Kutakuwa na mkutano wa waandishi wa Habari siku moja kabla ya mchezo ambapo Kocha Mkuu na Nahodha au mchezaji mwenye Ushawishi ndani ya Timu yake watazungumza katika mkutano huo.

Maboresho ya Kanuni

Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) ndani ya kipindi cha mwezi Mei iliendelea na mchakato wa maboresho ya Kanuni za Ligi kwa toleo la mwaka 2026 kwa kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali wa mpira wa miguu nchini.


Mchakato huo uliozinduliwa rasmi Aprili 22, 2026, ulihusisha ukusanyaji wa maoni kuhusu Kanuni za Ligi Kuu, Championship na First League, ukiwalenga wadau wote wakiwemo klabu , viongozi wa mpira wa miguu, waamuzi, makocha, wachezaji, maafisa habari pamoja na wadau wengine wa mpira wa miguu.

Katika kipindi hicho, TPLB ilipokea maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha uendeshaji wa ligi, kuimarisha ushindani, kuongeza uwazi katika maamuzi na kutatua changamoto zilizojitokeza pamoja na zinazoweza kujitokeza katika misimu ijayo.

Bodi inaushukuru ushiriki mkubwa ulioonyeshwa na wadau na viongozi mbalimbali waliojitokeza kutoa maoni yao. Ushirikishwaji huu ni sehemu muhimu ya kuhakikisha kuwa kanuni zinazotumika zinakidhi mahitaji ya sasa ya maendeleo ya mpira wa miguu na uendeshaji wa ligi nchini.

TPLB inaendelea kuyafanyia kazi maoni yote yaliyowasilishwa kwa lengo la kuandaa kanuni bora zaidi zitakazochangia maendeleo ya ligi na mpira wa miguu wa Tanzania kwa ujumla.









Picha mbalimbali za kamati ya maboresho ya Kanuni inayoundwa na Serketarieti ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania wakiwa wamekutana na makundi mbalimbali wakati wa ukusanyaji wa maoni





azamtv

MECHI 104 MAGIFTI 104 SABABU 104 ZA KUSHEREHEKEA!

MSHINDI NI WEWE!

KILA MECHI = MSHINDI MMOJA



Tazama Mechi za Kombe la Dunia 2026 Mbashara Katika AzamTV

Piga Picha au Video, kisha share kwenye mitandao ya kijamii

@ TAG
@azamtvtz
@azamtvsports
@azamtvmaxapp

Tumia #VibeNaAzam



SHIRIKI NA USHINDE VIFURUSHI VYA MIEZI 2 VYA JUU VYA AZAMTV

KILA MSHINDI ATAUNGANISHWA NA VIFURUSHI VYA MIEZI 2 KILA MECHI YA KOMBE LA DUNIA

